# UKALIMANI KATIKA MAHUBIRI KANISANI: UPOTOSHI AU UPANUZI WA MAANA?

**Moses Wamalwa Wasike[1], Mark Mosol Kandagor[2], na Magdaline Nakhumicha Wafula[3]**

[1]Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret – mmwasike@gmail.com
[2]Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret – mosolkandagor@gmail.com
[3]Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret – mnwafula@gmail.com

**Ikisiri**

*Makala hii inachunguza mchango wa dini katika lugha ya Kiswahili. Mchango wa dini katika maisha ya binadamu huwamba nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Dini imekuwa na nafasi muhimu katika maendeleo ya Kiswahili, hasa kupitia tafsiri na ukalimani, tangu enzi za ukoloni na ujio wa Wamishonari. Ukalimani wa kijamii, hususan katika mahubiri, huathiri Kiswahili ama kwa kukikuza au kukidumaza kimsamiati na kisarufi. Wakati mwingine, mkalimani hukosa muda wa kupitia na kusahihisha tafsiri yake, na kuleta tafsiri isiyokusudiwa. Mbali na umilisi wa lugha chanzi na pokezi, tafsiri humhitaji mfasiri kusomea tafsiri. Kwa hiyo, ukosefu wa muda hauwezi kuwa idhini kwa mkalimani kutepetea kwa sababu ujumbe unaokusudiwa na mzungumzaji ndio huwa muhimu zaidi. Mahubiri yanapokalimaniwa, lugha hutumiwa kiholela, na wakati mwingine inabadilisha maana inayokusudiwa. Lengo la makala hii ni kubainisha matumizi maalum ya lugha katika tafsiri za kidini, kutathmini iwapo matumizi hayo yanapanua au kupotosha Kiswahili kimsamiati na kimaana, na kutoa mapendekezo yatakayoboresha ukalimani wa mahubiri ya kidini ili kuchangia ukuaji wa lugha ya Kiswahili. Uchunguzi umejikita katika makanisa ya kiroho mjini Kakamega ambako mahubiri yalisikilizwa na kurekodiwa katika miktadha yake ya asili. Katika utafiti huu, data zilikusanywa kwa njia ya usikilizaji na kurekodi mahubiri katika miktadha yake ya asili. Kisha, muundo wa kimaelezo ulitumika kuchanganua data ili kutoa uelewa wa athari za ukalimani katika maendeleo ya Kiswahili.*

**Dhana za Msingi:** Usemi Asilia (UA), Usemi Tafsiri (UT), Matini Chanzi (MC), Matini Lengwa (ML), Ukalimani, Tafsiri, Fasiri.

## 1.0 Utangulizi

Wanjala (2002) na Mshindo (2010) wanasema ukalimani ni shughuli ya kiakili inayowezesha kuwasiliana kwa maneno yaliyosemwa au ishara zinazoonyeshwa baina ya watu ambao hawasemi lugha moja au ambao hawatumii ishara za aina moja. Ukalimani ni kuhawilisha

ujumbe ulioko katika mazungumzo, pamoja na uamilifu wake, kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa kuzingatia isimu, utamaduni na muktadha wa jamii husika.

Kuna aina kuu mbili za ukalimani: Ukalimani wa papo kwa papo na ukalimani fuatizi. Wa papo kwa papo hutokea pale ambapo msemaji wa MC na msemaji wa ML hupishana kwa muda kidogo sana (Wanjala, 2002). Si rahisi msikilizaji kuhisi kuwa mkalimani husikiliza kabla ya kuyatafsiri aliyoyasikia kwa sababu sauti ya msemaji katika lugha chanzi haipishani kabisa na sauti ya msemaji katika lugha lengwa. Ukalimani wa papo kwa papo humpasa mkalimani awe na uwezo na ujuzi wa hali ya juu. Ukalimani wa aina hii hutumika sana katika mikutano ya kimataifa, mihadhara ya kidini na pia katika mahakama za kimataifa.

Ukalimani fuatizi msemaji wa MC na msemaji wa ML hupishana kwa kipindi kirefu katika usemi. Kwa mujibu wa Wanjala (2002), hadhira hutambua wazi kwamba kuna wasemaji wanaozungumza kwa kupokezana zamu. Msemaji wa MC husema kwa kituo ili kumpa nafasi msemaji wa lugha lengwa kufafanua kwa lugha ya ML. Upokezanaji zamu huo unaweza kuwa kila baada ya sentensi, aya au hata matini nzima alimuradi mkalimani anapewa nafasi kujitayarisha. Mfumo huu wa ukalimani hujitokeza sana katika mahubiri ya kidini na wakati mwingine kwenye mikutano ya kisiasa.

Fauka ya ukalimani kuwa taaluma na nyenzo ya mawasiliano yenye ukati katika maenezi ya dini, maendeleo, umoja baina ya jamii lugha tofauti, amali za jamii na tamaduni mbalimbali duniani, ni nyenzo muhimu ya kufunza na kujifunzia lugha. Kwa mujibu wa Biamah (2013) na Ireri na wenzake (2012), mahubiri ni njia adhimu ya kujifunza na kufundisha lugha. Waumini wengi wakiwamo watoto huwachukulia wahubiri wao kuwa walio katika kiwango na hadhi ya juu kuliko watu wa kawaida. Lugha ya maabadini hufikiriwa na wengi kuwa ndiyo sahihi na sanifu na kwa hiyo ni mfano wa kuigwa. Wanayoyatenda na kuyasema viongozi wa maabadini huchukuliwa kuwa ukweli wa msahafu.

Ireri na wenzake (2012) wanatoa mfano wa madhehebu makuu ya kidini duniani; Uislamu, Katoliki na Anglikana ambayo waumini au wafuasi wake huchukulia mawasiliano katika mafundisho ya kidini kwa udhati na uzingativu. Wanadahili kwamba lugha na sheria zake huzingatiwa na kupewa uzito kwa muda mrefu sana katika mtaala wa mafunzo kwa makasisi. Hii

ni kutokana na taasisi hizo kutambua kuwa makasisi wao huchukuliwa na waumini kama vielelezo katika nyanja zote za maisha ikiwemo lugha na mawasiliano. Hivyo basi, umilisi wao wa lugha za mahubiri hupewa kipaumbele ambapo wao hutarajiwa kuzungumza, kuandika, kukalimani na kutafsiri kwa ufasaha.

Tangu enzi za ukoloni, madhehebu makuu ya Kikristo - Katoliki na Anglikana - yamekuwa yakisisitiza matumizi ya lugha za kiasili kwa kuwatumia wahubiri wanaoelewa lugha za kiasili za maeneo husika (Biamah, 2013). Hii imefanya utegemezi kwa wakalimani kuwa mdogo. Kwa upande mwingine, madhehebu ya kiroho huwaruhusu wahubiri wasio na uwezo wa kuzungumza lugha za kiasili kuhubiri na kutumia wakalimani kufikisha ujumbe. Wakati mwingine, ukalimani umepewa kipaumbele sana kiasi cha wahubiri wanaoelewa lugha za kiasili kustahabu kutumia Kiingereza kisha mahubiri yao kukalimaniwa. Tofauti na tafsiri ya kimaandishi, mkalimani huhitaji kuelewa kwa haraka, maana ambazo maneno yanaweza kueleza katika miktadha mbalimbali kisha aweze kuhamisha maana hizi katika ML (Oluoch, 2014). Ukalimani hufanywa papo hapo pasipo na nafasi ya kutosha ya kurekebisha makosa. Ni katika mchakato huu wa ukalimani ambapo makosa ya kimsamiati, kisarufi na kimaana hujitokeza na kupotosha ujumbe.

Suala hili ndilo lililowachochea watafiti kuuzamia uwanja huu ili kubainisha hali ilivyo nyanjani kwa kutumia mahubiri ya makanisa ya kiroho mjini Kakamega. Makala hii imebainisha makosa katika lugha ya ukalimani, kudhihirisha vyanzo vya makosa hayo na kupendekeza mbinu za kurekebisha hali hizo. Maneno ‘fasiri’, ‘tafsiri’, na ‘kalimani’ yametumiwa kama visawe katika makala kwa maana ya kuhawilisha mawazo yaliyo katika usemi wa mazungumzo kutoka lugha moja hadi nyingine.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozalisha makala hii uliongozwa na Nadharia ya Tafsiri ya Kikalimani (*Interpretive Theory of Translation*) ya Marianne (2003). Kwa mujibu wa nadharia hii, mchakato wa tafsiri unahusisha uelewaji wa ujumbe kutoka kwa MC, ufasiri (ukalimani) kisha kupitisha ujumbe huo ulivyoeleweka kwa hadhira. Maana yake ni kwamba tafsiri itekelezwe kwa misingi ya uhawilishaji wa maana kwa maana bali si neno kwa neno. Nadharia hii inazingatia michakato ya

kiakili na kiutambuzi inayohusika katika tafsiri ya maneno ya kiusemi na maneno ya kimaandishi ambayo ni: kuelewa matini husika, kugeuza lugha yake na kuwasilisha maana.

Nadharia hii ilifaa sana utafiti huu kwa sababu inashadidia hali kuwa ni muhimu kwa mkalimani kufasiri maana ya maneno ya mhubiri na kuiwasilisha dhana au maana hiyo kwa hadhira kuliko kujaribu kutafsiri neno kwa neno. Ni katika mizani hii basi ndipo utafiti ulibainisha kuwa upotoshi mwingi wa kimaana ulioshuhudiwa katika mahubiri yanayohusisha Kiingereza hadi Kiswahili katika makanisa ya kiroho mjini Kakamega yanatokana na tafsiri ya neno kwa neno. Kwa jumla, makala hii inahitimisha kuwa uelewaji wa maana ya usemi wa mhubiri kisha kuwasilisha maana au ujumbe huo ulivyoeleweka na mkalimani kwa hadhira ni mkakati bora wa kupunguza upotoshi wa kitafsiri.

## 3.0 Muundo wa Utafiti

Utafiti uliozalisha makala hii ulichukua muundo wa kimaelezo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Utafiti ulifanywa katika makanisa matano ya kiroho mjini Kakamega. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumiwa kuteua makanisa matano ambapo mahubiri hutolewa katika Kiingereza na kukalimaniwa kwa Kiswahili. Mahubiri ya kila kanisa yalihudhuriwa mara mbili. Jumla, kulikuwa na mahudhurio kumi ya mahubiri. Kutokana na haja ya kuheshimu haki za wakalimani (Milroy, 1987), watafiti waliwafahamisha wasimamizi wa makanisa haya kuhusu ziara yao ya utafiti. Mahubiri yalisikilizwa katika miktadha yake asilia. Mahubiri yalirekodiwa kwenye kinasa sauti bila kujulisha wahubiri na wakalimani. Mahojiano yalifanywa na wakalimani watano wa makanisa haya baada ya mahubiri. Watafiti walibainisha na kuandika wakati wa mahubiri pamoja na makala za sauti zilizorekodiwa kanisani vipande vya ukalimani visivyofasiriwa kwa usahihi kisha kuvitolea fasiri sahihi.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti na Mjadala

Makala hii inachunguza makosa katika viwango vya ukurubishaji wa msamiati kimaana, uziadafafanuzi wa kimsamiati, ubadilishaji wa msamiati unaokaribiana kimatamshi, tafsiri kisarufi na tafsiri ya semi.

### 4.1 Ukurubishaji wa Msamiati Kimaana

Mbinu ya matumizi ya msamiati unaokaribiana kimaana inavyotumika katika nadharia ya tafsiri ni uteuzi na upachikaji wa neno ambalo linakaribiana kimaana na neno linalotafsiriwa. Neno hili hutoa kwa hadhira, fununu kuhusu dhana inayorejelewa katika muktadha wa usemi asilia. Tarone (1983) anasema kuwa ukurubishaji ni matumizi ya neno la lugha lengwa lililo na sifa za kisemantiki zinazokaribiana na neno la lugha asilia. Anasema kuwa msamiati wa lugha lengwa unaoteuliwa na mkalimani huwa si mwafaka lakini kimuktadha, unapatikana katika uwanja mmoja wa fahiwa pana kisemantiki na msamiati husika wa lugha asilia. Hali hii ama hugeuza au hupotosha maana kusudiwa ya usemi asilia. Upotoshi huu unajitokeza katika mifano ifuatayo:

**Mfano wa 1**: UA: *We pray that God* ***forgives us*** *our sins*.

UT: Tunaomba kuwa Mungu **atuhurumie** dhambi zetu.

Neno **huruma** hapa limetumiwa kimakosa. Kwa mujibu wa BAKITA (2015), neno **huruma** lina maana ya kuwa na moyo au hisia za kusaidia wengine. Huruma huelekezwa moja kwa moja kwa kitu chenye uhai au hisia. Hivyo, dhambi hazihurumiwi. Neno mwafaka lilifaa kuwa **atusamehe, atuondolee** au **atughofirie**. **Ghofiri** likiwa ndilo mwafaka kwa vile linarejelea uwezo ambao Mwenyezi Mungu pekee yake anao kuhusu kuondolea binadamu dhambi. Mkalimani amelipatia neno hili maana nyingine isiyofaa kwa kutumia ukurubishaji wa **samehe** na **hurumia**, maneno yanayopatikana katika fahiwa ya maneno tangamani. Maneno tangamani kwa mujibu wa Halliday na Hassan (1976), ni yale yanayoakisi ushikamano wa kimsamiati unaohusu mjumuisho wa maneno ambayo yanaweza kutokea pamoja. Wanasema kuwa, baadhi ya maneno hutokea pamoja mara kwa mara kuliko mengine. Kwamba tunapotaja neno moja, kwa kawaida huwa linaibua neno jingine katika akili ya msikilizaji ambaye atalihusisha na lile la kwanza. Wanatoa mifano ya maneno yaliyo katika seti moja isiyo na mpangilio maalum na hiponimu jumuishi zilizo katika kundi moja. Mathalani, msamaha-huruma (hisia), ukali-hasira (hisia), kiti-meza (samani), mbuzi-kondoo (wanyama). Kila neno hujulikana kutokana na maneno mengine yanayoendana nalo. Hata hivyo, wanasema maneno haya hayafai kuchukuliwa kama visawe. Ni maneno yaliyo katika mkufu mmoja wa maana lakini hayawezi kutekeleza kazi moja kisemantiki.

Hivyo basi, upanuzi wa maana ambao unaweza kuwa ulikusudiwa na mkalimani katika muktadha huu hauafiki hali kwani tayari kuna msamiati mwafaka na wa kutosha unaofaa kutumiwa au kurejelea hali hii. Hali hii inapotosha hadhira kuhusu maana ya maneno husika. Ifuatayo ni mifano zaidi:

**Mfano wa 2.** UA: *We were created from* ***soil*** *and ultimately, we will end up becoming* ***soil*** *again*.

UT: Tuliumbwa kutoka kwa **mchanga** na mwishowe tutaishia kuwa **mchanga** tena

Mkalimani amelipa neno **mchanga** maana mpya ambayo si sahihi. BAKITA (2015) linafafanua neno **mchanga** kuwa udongo wenye chembechembe ndogo za mawe. Ni udongo wenye chembechembe laini sana za mawe yaliyosagika. Mchanga ni aina ya udongo usio na masalia ya mimea na wanyama ambayo huwezesha mimea kuota na viumbe kuishi. Ingawa maneno haya yanakaribiana kimaana, neno **udongo** ni la jumla huku **mchanga** ukiwa ni aina ya udongo. Neno **soil** au **earth** hurejelewa kama **udongo** katika Kiswahili na **sand** hurejelewa kama **mchanga** katika Kiswahili. Hivyo basi, neno mwafaka lililofaa kutumiwa lilikuwa **udongo**, sio **mchanga**

Katika mbinu ya upanuzi wa maana kwa mujibu wa Kiango (2004), maana ya awali ya neno hupanuliwa na kuhusishwa na maana nyingine. Hata hivyo, njia hii hutumiwa tu panapo haja ya kukidhi dhana ambazo awali hazimo katika utamaduni na msamiati wa lugha husika. Katika tafsiri zinazojitokeza katika mifano 1 na 2 hapo juu, ingawa maneno husika yanapatikana katika uwanja mmoja wa fahiwa pana kisemantiki, maana iliyolengwa na msemaji imegeuzwa. Matumizi holela ya msamiati unaokaribiana kimaana na msamiati mwafaka yanashuhudiwa. Hali hii inapotosha maana kusudiwa ya mhubiri na kuwasilisha maana nyingine tofauti kabisa.

## 4.2 Uziada-Fafanuzi Potoshi wa Kimsamiati

Hii ni mbinu ya kuongezea maneno yasiyohitajika, yasiyo ya lazima, yasiyoongeza jambo jipya, yasiyoongeza taarifa mpya bali kupotosha maana katika ML (Smit, 1999). Grice (1975) na Levinson (1983) wanatoa mchango wao kwa kusema kuwa katika mawasiliano mtu asitoe habari zaidi ya inavyohitajika. Kwamba mtu atoe tu kiasi kitakikanacho cha taarifa na aepuke maelezo mengi yasiyo ya lazima. Katika baadhi ya tafsiri mkalimani anatoa habari za ziada ambazo

hazipo katika MC. Mbinu ya uziada-fafanuzi huchukuliwa kama upanuzi potoshi wa maana ambapo mkalimani hunuia kuufanya ujumbe unaotolewa kuwa wazi zaidi. Msamiati wa ziada hausaidii kujaliza maana ya msamiati uliotumiwa. Uziada huu aghalabu unazua maana ambayo si sahihi kimantiki.

**Mfano wa 3:** UA: *You will get **blessings** for your good deeds*.

UT: Utapata **baraka *njema*** kutokana na matendo yako mazuri.

Neno **njema** linazua dhana ya kuwa kuna baraka njema na baraka mbaya, hali ambayo si halisi. Maana ya neno **baraka** ni jumla ya mambo yote mazuri katika maisha ya mtu. Ufafanuzi huu ni kwa mujibu wa (BAKITA, 2015). Kwa hivyo 'wema' umekwishafumbatwa katika maana ya neno 'baraka'. Kuongezea neno **njema** hakupanui maana ya neno hili ila kunazua upotoshi. Mkalimani alifaa tu kutumia neno **baraka**.

**Mfano wa 4:** UA: *As Christians, we must uphold **morals** of the society*.

UT: Kama Wakristo, tunafaa kudumisha **maadili *mema***.

Neno **mema** halipanui maana ya neno **maadili** bali linapotosha. Linazua hali kwamba kuna maadili mema na mabaya ingawa hakuna hali kama hiyo. Kutokana na maelezo ya BAKITA (2015), neno **maadili** maana yake ni tabia yenye kukubaliana na mielekeo bora katika jamii; mwenendo *mzuri*, wa kupendeza, unaokubalika na kufurahisha. Ni maelekezo *mazuri* yanayotolewa ili kuboresha tabia na mwenendo wa mtu katika kazi au maisha. Kwa hivyo, katika maana ya maadili, kuna dhana ya *uzuri* ambayo haihitaji uziada wa kufafanuliwa na neno jingine. Mkalimani alifaa kusema tu **maadili** bila kuongeza neno **mema**.

**Mfano wa 5.** UA: ***My** dear brethren…*

UT: Ndugu **zanguni** wapendwa…

Kiambishi – **ni** cha nafsi ya pili katika wingi kimepachikwa kimakosa kwenye kivumishi kimilikishi – **angu.** Kiambishi hiki huongezwa kwenye vitenzi na vihisishi tu bali si kategoria nyingine za maneno. Mathalani, kwenye maneno *kuje-**ni*** (kitenzi) na *karibu-**ni*** (kihisishi)

kiambishi -**ni** kinaleta dhana ya wingi wa warejelewa. Ili kuleta dhana ya wingi wa warejelewa kwenye mzizi milikishi **-angu**, kiambishi **z-** cha ngeli katika wingi kimechukua nafasi ya kiambisha **y-** cha ngeli katika umoja. Hivyo basi, kuongeza kiambishi **–ni** uziada na kosa la kisarufi. Huu si upanuzi wa maana ya neno bali ni upotoshi kisarufi.

Kwa mujibu wa Smit (1999), licha ya mbinu ya uziada-fafanuzi kusaidia kuelewesha zaidi hadhira kuhusu ujumbe ulionuiwa na msemaji, aghalabu huwa ni upotoshi kisarufi na kimantiki. Badala ya kusoza wakati kwa kutoa maelezo na habari ambazo hazipo kwenye MC, mkalimani anafaa kuutumia wakati huo kusikiliza kauli ya msemaji inayofuata na kuandaa tafsiri yake mwafaka. Smit (ameshatajwa) anadai kuwa mbinu hii haifidii upungufu wa mkalimani katika tafsiri.

### 4.3 Ubadilishaji wa Msamiati Unaokaribiana Kimatamshi

Kosa la matumizi ya maneno yanayokaribiana kimatamshi lilijitokeza katika tafsiri za kanisani. Mkalimani alikosa kutofautisha kati ya jozi finyu ya msamiati na kuutumia msamiati mmoja kama kibadala au kisawe cha mwingine katika usemi tafsiri.

**Mfano wa 6:** UA: Righteous men relish a unique spiritual **environment** in the earthly section of Jehovah's system.
UT: Watu waadilifu hufurahia **mazingara** ya kipekee ya kiroho duniani katika mfumo wa Yehova.

**Mfano wa 7:** UA: Of Jesus's twelve disciples, Peter was one of his most **powerful** apostles.
UT: Miongoni mwa wafuasi kumi na wawili wa Yesu, Peter alikuwa mojawapo ya watume wake **hatari** sana.

Kwa mujibu wa Matinde (2012) akimnukuu Trubetzkoy (1969), kigezo cha Mpishano Huru katika fonetiki hutokea pale ambapo sauti mbili zinaweza kutokea katika mazingira yale kwa kubadilishana bila kusababisha mabadiliko ya maana ya neno. Katika hali hii, sauti hizo huitwa vibadala huria au vibadala vya hiari vya kifonetiki. Mathalani, maneno '**suala**' na '**swala**' yanachukuliwa kama vibadala. Vibadala hivi vinaonekana kuwa ni sauti za fonimu moja isipokuwa kwamba kibadala '**suala'** huchukuliwa kuwa ni utamkaji sanifu (mzuri) na kibadala

'swala' huchukuliwa kuwa ni mkengeuko wa kilahaja, kijamii (sifa, umaarufu, umjini) au kimaumbile (Mulikuza, 2023). Hata hivyo, yote yanakubalika kutumiwa kurejelea neno 'jambo.'

Katika muktadha ya maneno '**mazingira**—**mazingara**' na '**hodari**—**hatari**', hakuna uhalali wa kuwa vibadala. Maneno haya yanarejelea dhana tofauti kabisa. Kulingana na sheria ya Jozi Mlinganuo Finyu, Matinde (2012 akimnukuu Trubetzkoy (1969), maneno mawili au zaidi yanakuwa na idadi sawa ya sauti na ubadilishaji wa sauti moja katika mazingira yale ya utokeaji wa kifonetiki wa sauti hizo katika neno huleta tofauti kimaana.

Trubetzkoy anasema kuwa ikiwa sauti fulani tofauti zitajitokeza katika neno hilo na katika mazingira yale ya kifonetiki na kubadili maana ya neno, basi zinachukuliwa kuwa fonimu mbili tofauti. Hivyo, maneno yanayohusika si visawe tena ila maneno tofauti yenye maana tofauti na bainifu. Ni msamiati wenye fahiwa tofauti kabisa zisizokaribiana. Kwa hiyo, maneno '**mazingara**' na '**hatari**' hayawezi kutumiwa kama vibadala au visawe vya '**mazingira**' na '**hodari'** mtawalia kurejelea dhana ya '*environment*' na '*powerful*' katika MC. Maneno '**mazingara**' na '**hatari**' tafsiri yake katika lugha asilia ni '**superstition'** na '**dangerous'** mtawalia. Badala ya dhana kusudiwa za 'eneo' (***environment***) na 'mwingi wa akili, maarifa, ujuzi, ujasiri na utaalamu' (***powerful***) maana tenge zinazojitokeza ni kuwa mfumo wa Mungu una ushirikina (**mazingara**) na Peter alikuwa tishio kwa usalama na angeweza kusababisha maafa, janga au ajali (**hatari**). Matumizi yake hivyo basi yalipotosha maana kusudiwa ya mhubiri kwa hadhira.

## 4.4 Upotoshi wa Kisarufi

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999) na Matinde (2012), sarufi ni kanuni, sheria au taratibu zinazotawala kila moja kati ya viwango vinne vya lugha ambavyo ni umbo-sauti (*fonolojia)*, umbo-neno (*mofolojia*), miundo-maneno (*sintaksia*) na umbo-maana (*semantiki*). Sarufi ni kanuni, sheria au taratibu zinazotawala lugha katika matumizi yake ambayo hujumuisha matamshi, maumbo, miundo na maana.

Kwa ujumla, sarufi inaweza kuelezwa kama kanuni, sheria na taratibu zinazomwongoza mzungumzaji au mwandishi kuzungumza au kuandika tungo sahihi zinazoeleweka kwa

msikilizaji wa lugha ileile. Matumizi ya lugha tafsiri yaliyokiuka kanuni za kisarufi yanadhihirika katika viwango mbalimbali ifuatavyo:

***Mnyambuliko Usiofaa wa Nomino Kuunda Vitenzi***

Kuna makosa ya kuongeza viambishi vya mnyambuliko kwenye nomino isivyofaa kisarufi.

**Mfano wa 8.** UA: *Avoid people who* ***obstruct*** *you from serving God*.

UT: Epukana na watu **wanaokukwaza** usiweze kumhudumia Mungu.

Neno ***obstruct*** kisawe chake katika Kiswahili ni **zuia** au **kuwa kikwazo**. Mkalimani amenyambua neno **kikwazo** ambalo ni nomino na kulifanya kitenzi. Haya ni makosa ikizingatiwa kuwa kuna msamiati faafu ambao ungeafiki hii hali kama vile **wanaokuzuia**. Vilevile, maelezo yangeafiki alipokosa neno moja la kuafiki neno la MC mathalani, **wanaokuwa kikwazo** au **wanaokuwa pingamizi**. Kazi ya mkalimani ni kuwasilisha ujumbe ulivyokusudiwa na msemaji kwa njia yoyote bila kupotosha maana. Yaweza kuwa kimaelezo au kwa msamiati wa visawe (Marianne, 2003).

**Mfano wa 9.** UA: *As a good Christian, you must* ***be responsible*** *to your family…because at the end*

*of the day, you will* ***be accountable*** *for your actions*.

UT: Kama Mkristo mzuri, lazima **ujukumikie** familia yako…kwa sababu *mwisho wa*

*siku* **utajukumikia** matendo yako.

Neno **jukumu** ambalo ni kisawe cha **wajibu**, limenyambuliwa kwa kuongezwa viambishi vya kauli kwa kufuata mtindo wa neno **wajibika** kutokana na neno **wajibu**. Inafahamika kuwa, si nomino zote hunyambuliwa katika Kiswahili ili kuunda msamiati mpya (Matei, 2008). Huu upanuzi wa maana ya neno **jukumu** unapotosha. Maneno mwafaka yalifaa kuwa **uwajibike kwa** au **uwajibikie** kwa maana ya ***be responsible*** na **utachukua dhamana** ya vitendo vyako kwa maana ya ***be accountable*** *for your actions*. Isitoshe, msemo ***end of the day*** umetafsiriwa

kimakosa. Kosa hili litaangaziwa baadaye katika kitengo kingine kwenye makala (tazama sehemu ya Tafsiri Mbovu ya Semi):

***Mwingiliano wa Maneno***

Mwingiliano wa maneno ni hali ya neno moja kuweza kubadili aina yake katika sentensi (Matei, 2008). Kwa mfano, kiwakilishi kinaweza kubadilika na kuwa kielezi au kihisishi na kadhalika. Ni hali ambapo kategoria moja ya neno huweza kubadili kategoria yake na kufanya kazi ya kategoria nyingine ya neno. Mathalani, kitenzi kinaweza kutumiwa kama nomino katika muktadha tofauti na nomino ikatumiwa kama kielezi katika muktadha tofauti. Mwingiliano tenge ufuatao ulidhihirika katika uchunguzi huu.

**Mfano wa 10.** UA: *Prayer is an* ***enough*** *resource to connect you with God*.

UT: Maombi ni rasilimali **tosha** ya kukuunganisha na Mungu.

Katika mwingiliano wa maneno, kategoria moja ya neno huweza kutumika katika mazingira tofauti ya sentensi na kufanya kategoria ya neno hilo kubadilika. Hata hivyo, si maneno yote huweza kutumika katika miktadha tofauti ya sentensi na kufanya kazi ya kategoria nyingine ya neno (Habwe na Karanja, 2012). Katika muktadha huu, neno **tosha** ni **kitenzi** ambacho kimetumiwa visivyo kuleta dhana ya kivumishi. Neno hili halibadilishi kategoria yake ya kitenzi na kufanya kazi ya kategoria nyingine ya neno. Hivyo basi, kupanua maana ya neno hili ili lifanye kazi ya kivumishi ni upotoshi wala sio upanuzi wa maana. Badala yake, kivumishi **toshelezi** au kirai kivumishi **ya kutosha** yangeliafiki zaidi.

***Uambishaji Mbaya wa Nomino***

Nomino za Kiswahili huwekwa katika makundi yanayoitwa ngeli kulingana na sifa za kimuundo, kisintaksia na kisemantiki. Kila kundi lina sifa zinazotambulisha nomino zinazoingizwa kwenye kundi hilo (Habwe na Karanja, 2012). Mathalani, kimuundo au kimofolojia, katika ngeli ya 1 {mu} na ngeli ya 2 {wa} nomino nyingi hutambulishwa kwa kuwa na mianzo ya kiambishi ngeli {mu} katika ngeli ya 1 na {wa}- katika ngeli ya 2. Hata hivyo, kuna nomino ambazo zina mianzo isiyofuata sheria hii. Upekee huu unazua utata wakati wa ukalimani ambapo wakalimani

hushadidia kufuata sheria ya mianzo ya {mu} na {wa} kwenye nomino zote zinazopatikana kwenye makundi haya ya ngeli inavyodhihirika kwenye mfano 11 ufuatao.

**Mfano wa 11.** UA: *All **fathers** and **mothers,** blaze the way of Christianity for your children to follow*.

UT: **Wababa** na **wamama** wote, angazeni njia ya Kikristo ili watoto wenu waifuate.

Nomino **baba** na **mama** zimeambishwa kimakosa kwenye tafsiri hiyo. Mkalimani alifuata mfumo wa ngeli ya 1 na 2 kimakosa na kuchukulia kuwa nomino hizi zinafaa kutanguliwa na viambishi {mu} na {wa} katika umoja na wingi na kuwa {mu+baba} → {wa+baba} na {mu+mama} → {wa+mama}. Kimofolojia, {mu} huwa {m} ikiwa shina la nomino linaanzia kwa konsonanti (Habwe na Karanja, 2012). Hivyo, matamshi ya '**mbaba** na '**mmama'** kama inavyoashiriwa na mkalimani yametokana na {mu+baba} na {mu+mama}. Nomino **baba** na **mama** ni mofu kapa ambazo hazichukui viambishi vya idadi katika umoja na wingi. Katika wingi, zilifaa kutanguliwa na mofu '**kina'** au '**akina'** ambazo hutumiwa kurejelea wingi wa nomino zinazowakilisha binadamu ambazo ni kapa. Hivyo, kosa hili halingejitokeza ikiwa mkalimani angelitamka '**akina baba**' na '**akina mama**' badala ya '**wababa**' na '**wamama.**' Kosa hili laweza kuwa lilitokana na mkalimani kutofahamu sheria za kisarufi au mapuuza kwa kutaka kurahisisha kazi yake.

### 4.5 Tafsiri ya Moja kwa Moja ya Semi

Okpewho (1992), Mulokozi (1996), na Mauya (2006) wanafasili semi kuwa fungu la maneno ambayo hupangwa kwa pamoja kisanii na kuleta maana isiyokuwa ya kawaida. Wanazigawa semi katika vipera vyake kama: methali, misemo, nahau, misimu, lakabu, vitanza ndimi, shirikina na mafumbo. Katika muktadha wa utafiti, semi zilizoshughulikiwa ni misemo na nahau tu.

Kwa mujibu wa Mbaabu (1995), ni makosa kutafsiri semi za lugha ya kwanza au lugha moja hadi nyingine moja kwa moja kutokana na hali kwamba semi hujikita katika utamaduni wa jamii husika. Newmark (1981) anasema kuwa semi haziwezi kutafsiriwa moja kwa moja. Semi hizi

lazima zitafutiwe visawe kimaana katika lugha pokezi. Iwapo hazipo kwenye lugha pokezi, basi zifafanuliwe kimaelezo kuliko kutafsiriwa neno kwa neno; hali itakayozua maana tofauti kabisa na iliyokusudiwa na semi asilia. Newmark anazidi kusema kuwa tafsiri ya semi moja kwa moja huzua ukosefu wa ulinganifu wa maana kati ya usemi asilia na pokezi. Ukosefu huu unasababishwa na mambo mengi kama vile tofauti za matumizi lugha kati ya lugha chanzi na lugha pokezi, mifumo ya kisarufi ya lugha hizo, mifumo ya kisintaksia na kisemantiki na kuwepo kwa dhana zinazotofautiana katika lugha hizo.

Tafsiri ya moja kwa moja ya semi ilidhihirika katika tafsiri kama inavyoonyeshwa katika mifano ya misemo na nahau hapa chini.

**Mfano wa 12.** UA: *As a good Christian, you must be responsible in your actions…because* ***at the***

***end of the day**, you will be accountable for your actions*.

UT: Kama Mkristo mzuri, lazima *ujukumikie* familia yako…kwa sababu **mwisho wa siku**, *utajukumikia* matendo yako.

**Mfano wa 13.** UA: *Vices that weaken the body and spirit are* ***smoking cigarettes****, drunkardness, adultery and fornication*.

UT: Maovu yanayodhoofisha mwili na roho ni kama vile **kunywa sigara**, ulevi, zinaa na mapenzi kabla ya ndoa.

**Mfano wa 14.** UA: *Moses spent* ***the better part of the day*** *in the mountain conversing with God*.

UT: Musa alichukua **kipande kizuri cha siku** mlimani akizungumza na Mungu.

Katika mifano hii, misemo na nahau za Kiingereza; ***at the end of the day***, ***smoking cigarettes*** na ***the better part of the day*** zimetafsiriwa kimakosa moja kwa moja kama **mwisho wa siku**,

**kunywa sigara** na **kipande kizuri cha siku** badala ya kutafutiwa visawe vya kidhana katika lugha pokezi ya Kiswahili. Aidha, nahau **kunywa sigara** inaonekana ni tafsiri ya moja kwa moja ya msemo wa lugha ya kwanza ya mkalimani ambayo ni lugha ya Kiluhya. Tafsiri ya semi hizi ilifaa kuwa **mwishowe** au **hatimaye** '**kuvuta sigara**' na '**muda mrefu**' mtawalia.

Wataalamu mbalimbali wanaona kwamba, methali, misemo na nahau husukwa na kutumiwa kulingana na utamaduni wa watu fulani. Kwa kawaida, semi hizi hujikita katika historia, imani, falsafa na mazingira ya watumiaji. Hivyo, inasikitisha kuona jinsi wafasiri wanavyofanya tafsiri sisisi ya tanzu hizi. Kuondokana na tatizo hili, la tafsiri sisisi, wapo pia wanaopendekeza kwamba kupatikane visawe vya kimuundo na pili, kupatikane visawe kuntu vya dhana au maana ya misemo.

## 5.0 Mapendekezo

Kwa mujibu wa utafiti, ilibainika kuwa katika ukalimani wa mahubiri, wakalimani hawakuwa na taarifa kuhusu ujumbe wa wahubiri. Hii hutokana na imani ya kidini kwamba mhubiri hawezi kufichua ujumbe mapema na anaweza kubadilisha ujumbe kulingana na mwongozo wa roho mtakatifu (Ogonda, 1998), hivyo kubadili maudhui ya mahubiri. Kutokana na hali hii ya ukosefu wa utaratibu, mkalimani hukosa fursa ya kujiandaa hasa na kupitia kazi yake kabla ya kuwasilisha. Kwa hiyo, kanisa na mkalimani wanaweza pia kushirikiana ili mkalimani apate ufahamu wa awali kuhusu ujumbe utakaozungumzwa. Hii itamwezesha kujiandaa vilivyo na kuboresha usahihi wa tafsiri. Iwapo mkalimani anaweza kufahamu kiunzi cha somo, majina ya wahusika, na maeneo muhimu, atakuwa na uwezo bora wa kuelewa muktadha wa ujumbe.

Zaidi ya hayo, mkalimani anahitaji kuelewa kiwango cha hadhira yake ili kuchagua msamiati unaooana na uelewa wao, na hivyo kuhakikisha kuwa ujumbe unafikishwa kwa usahihi. Mkalimani anapozungumza na hadhira yenye elimu ya msingi, anapaswa kutumia maneno rahisi na mifano inayotokana na mazingira yao ya kila siku. Kwa mfano, ikiwa anahutubia watu wenye elimu ya juu, anaweza kutumia maneno ya kitaaluma na mifano ya kihistoria au ya falsafa.

Mkalimani anafaa kujiuliza maswali kadhaa kabla ya kuingia ulingo wa ukalimani. Mojawapo ya maswali ni kama vile: Je, kiwango cha elimu, umri na jinsia ya hadhira yangu ni gani? Kwa

mfano, ikiwa anatafsiri kwa wazee, anaweza kutumia misemo ya Kiswahili yenye hekima swali jingine ni: Mtazamo na matarajio yao ni yapi? Ikiwa anawasiliana na kundi la vijana wa kizazi cha dijitali, anaweza kutumia mifano kutoka kwa teknolojia na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha ujumbe unawafikia kwa ufanisi. Ufahamu wa majibu ya swali hili utamwezesha kuteua msamiati mwafaka unaooana na kiwango cha wasikilizaji wake, hivyo kuepuka tafsiri zinazoweza kuwa na makosa ya muktadha au kupotosha maana halisi ya ujumbe unaotolewa

Hatimaye, wahubiri na wakalimani wanafaa kutanabahishwa kuwa kuna makosa na upotoshi mwingi katika mahubiri yao kutokana na ukalimani mbovu. Kwa mfano, kuna wakati mkalimani anaweza kutumia neno lenye maana pana au potofu, jambo linaloweza kuathiri uelewa wa waumini. Katika baadhi ya makanisa, neno **neema** limewahi kutafsiriwa kama **bahati**, hali inayopotosha maana yake halisi ya kibiblia inayohusiana na fadhila za Mungu zisizo na masharti.

Hili litawafanya kumakinika zaidi katika kazi yao ili kupunguza makosa katika mawasilisho yao. Ikiwa wahubiri na wakalimani wataelewa uzito wa jukumu lao, watajitahidi kuhakikisha kuwa tafsiri zao ni sahihi na zinaendana na muktadha wa dini na imani. Kwa mfano, katika mahubiri yanayozungumzia **kutubu**, mkalimani anapaswa kutofautisha kati ya **kuomba msamaha** na **kutubu dhambi**, kwa kuwa maneno haya mawili yana maana zinazotofautiana kidogo katika maandiko ya kidini. Pia, wakalimani wanapaswa kuepuka tafsiri za moja kwa moja za methali au nahau ambazo zinaweza kupotosha maana. Kwa mfano, msemo wa Kiingereza **born again** umetafsiriwa visivyo na baadhi ya wakalimani kama **kuzaliwa mara ya pili** badala ya **kuokoka**, hali inayoweza kuchanganya waumini wasio na ufahamu wa kina wa lugha ya Kiingereza.

## 6.0 Hitimisho

Katika utafiti uliozalisha makala hii, iligunduliwa kuwa wakalimani aghalabu hutumia mbinu ya ukurubishaji kimaana wa msamiati unaopatikana katika uwanja mmoja wa fahiwa pana kisemantiki na msamiati husika wa lugha asilia. Mbinu hii huishia kugeuza au kupotosha maana kusudiwa ya usemi asilia. Aidha, wakalimani hutumia mbinu ya uziada-fafanuzi kusaidia kuelewesha zaidi hadhira kuhusu ujumbe ulionuiwa na msemaji. Pia, wao huitumia kufidia upungufu wao katika tafsiri kwa kutoa maelezo ya ziada ambayo hatimaye hupotosha ujumbe unaojitokeza.

Halikadhalika, wakalimani wanatumia maneno yenye kukaribiana kimatamshi kwa dhana kuwa maneno hayo yana sauti ambazo ni vibadala huria au vibadala vya hiari vya kifonetiki na hivyo yana maana moja. Machukulio haya kimakosa, yanageuza maana kusudiwa na kuwasilisha nyingine tofauti kabisa. Minghairi ya hayo, upotoshi wa maana ulijitokeza katika viwango vya kisarufi vya kunyambua nomino visivyofaa ili kuunda vitenzi, matumizi mabaya ya kategoria moja ya neno kufanya kazi tofauti ya kategoria nyingine pamoja na uambishaji mbovu wa nomino katika muktadha wa upatanisho wa kisarufi katika umoja na wingi.

Isitoshe, ilidhihirika kuwa semi (misemo na nahau) hutafsiriwa moja kwa moja bila kuzingatia utamaduni na maana katika lugha lengwa. Maana inayojitokeza inakuwa tofauti kabisa na maana asilia. Ni machukulio ya wengi kuwa tafsiri ya neno kwa neno ni mbinu nzuri ya kuhifadhi ujumbe asilia wa lugha chanzi katika tafsiri. Hata hivyo, utafiti huu umebainisha kuwa mbinu hii hupotosha ujumbe ulionuiwa na msemaji huyo.

**Marejeleo**

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Biamah, J. (2013). Dealing with communication challenges during interpretation of church sermons in Uasin Gishu County, Kenya. *International Journal of Humanities and Social Science, 3*(14), 148-157.

El Shiyab, S. (1994). Translation of text and context. *Babel, 40*(4), 232-238.

Grice, H. P. (1975). Logic and conversation. In P. Cole & J. Morgan (Eds.), *Syntax and Semantics* (Vol. 3, pp. 41-58). New York: Academic Press.

Habwe, J., & Karanja, P. (2012). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Halliday, M., & Hasan, R. (1976). *Cohesion in English*. London: Longman.

Ireri, H. K., Muriungi, P. K., & Waita, N. (2012). Misinterpretations in English-Kimuthambi Church Sermons. *English Linguistics Research*, 1(2).

Kiango, J. (2004). Uundaji wa Msamiati Mpya katika Kiswahili: Zoezi lenye njia mbalimbali. In *Kioo cha Lugha, 1*(1). Dar es Salaam: TUKI.

Levinson, S. (1983). *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Marianne, L. (2003). *The interpretive model*. Manchester: St Jerome.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y., & Mohideen, M. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (*SAMIKISA*): *Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A. (2008). *Darubini ya Sarufi*: *Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia*: *Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.

Mauya, A. B. (2006). *Semi*: *Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Milroy, L. (1987). *Observing and Analysis of Natural Language*: *A Critical Account of Sociolinguistic method*. Oxford: Basil Blackwell.

Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Kenya Ltd.

Mpemba, T. (2013). Hali ya taaluma ya ukalimani Tanzania: Jana, leo na kesho. *Kiswahili*, *76*, 111–139..

Mshindo, H. B. (2010). *Kufasiri na Tafsiri*. Zanzibar: Kiwanda cha Uchapaji Chuo Kikuu cha Chukwani.

Mulikuza, P. (2023). *Kutathmini athari za lugha ya Kisukuma katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri isiyochapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: OSW 105*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Newmark, P. (1981). *Approaches to Translation*. New York: Pergamon Press.

Ogonda, J. (1998). Matatizo ya Ukalimani: Uchambuzi wa Mahubiri ya Kidini. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Okpewho, I. (1992). *African oral Literature*. USA: Indiana University Press.

Oluoch, J. S. (2014). Uchanganuzi wa Kiamali wa Ukalimani wa Sitiari za Dini ya Kikristo kutoka Kiluo hadi Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Shekinyashi, M. (2018). Tafsiri na Ukalimani. Ilipakuliwa kutoka https://www.slideshare.net (20/08/2019).

Smit, H. (1999). Interpreting services in the pharmacy of the Kalafong Hospital in South Africa. In M. Erasmus (Ed.), *Liaison interpreting in the community* (pp. 165–174). Pretoria: Van Schaik Publishers.

Tarone, E. (1983). Some thoughts on the notion of communication strategy. In C. Faerch & G. Kasper (Eds.), *Strategies in interlanguage communication* (pp. 61–74). London: Longman.

Wanjala, F. S. (2002). *Misingi ya ukalimani na tafsiri: Kwa shule, vyuo na ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Limited.